



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - MIPANGO NA UWEKEZAJI
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC)



Unapojibu tafadhali taja :

Kumb. Na.CA.148/234.01. D/196

03 Aprili, 2025

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni,
S.L.P 31902
DAR ES SALAAM

**YAH: KUOMBA UTHIBITISHO WA UMILIKI KIWANJA NA. 84 ENEO LA VIWANDA
MBEZI- MANISPAA YA KINONDONI**

Kichwa cha habari hapo juu chahusika.

- Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimepokea maombi kutoka kwa kampuni ya YI MING INVESTMENT COMPANY LIMITED, ya kusajili mradi wa kiwanda cha kuchakata taka (Recycling) kwa ajili ya kupata Cheti cha Vivutio vya Uwekezaji (*certificate of incentive*). Kampuni imeambatanisha Mkataba wa mauziano wa kiwanja hicho baina yake na EVALYNE JOSEPH MBUNA, FOSTER IRENE MBUNA MKAPA AND FELICIA JOSEPH MBUNA.
- Ili TIC iendelee na taratibu za kusajili mradi, tunaomba ofisi yako itoe uthibitisho wa umiliki pamoja na matumizi ya ardhi ya kiwanja Na. 84 eneo la viwandani Mbezi -Manispaa ya Kinondoni yenye Hati Miliki Na.45471.
- Aidha, Uwekezaji huu ni muhimu sana katika Wilaya yako hivyo kulingana na Kifungu cha 18 (4) cha Sheria ya Uwekezaji, 2022 ambacho kimetoa sharti la maombi ya wawekezaji yanayotoka TIC yapatiwe mrejesho ndani ya siku saba za kazi, naomba kuwasilisha maombi haya kwa hatua zaidi.
- Nashukuru kwa ushirikiano.

J. A. Haule

Kny: MKURUGENZI MTENDAJI

Nakala: Mkurugenzi
Yi Ming Investment Company Limited
S.L.P 80679
DAR ES SALAAM



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. KMC/LD/25165/KVK

10/04/2025

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania,
S.L.P. 938,
DAR ES SALAAM.



Yah: **UTHIBITISHO WA UMILIKI WA KIWANJA NA. 84 ENEO LA VIWANDA MBEZI
MANISPAA YA KINONDONI**

Ofisi inakiri kupokea barua yako ya tarehe 03/04/2025 ikiwa na Kumb Na. C.A.148/234.01.D/196.

2. Kwa barua hii unajulishwa kwamba ofisi yetu haina kumbukumbu za umiliki wa kiwanja hicho kwa sababu milki hiyo inaonekana ilitolewa na kushughulikiwa na ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Dar es salaam.
3. Kwa muktadha huo kumbukumbu za milki hiyo zinapatikana katika ofisi hiyo. Pamoja na hayo unashauriwa kuomba kumbukumbu hizo na taarifa katika ofisi ya Msajili wa Hati Mkoa wa Dar es salaam kwa sababu milki hiyo imesajiliwa.

Naomba kuwasilisha.

Kipeta K.

Kny: **MKURUGENZI WA MANISPAA**